

Sifa za Vitanzandimi vya Kiswahili katika Mawasiliano ya Jamii

Rashidi Abdallah Mwanyumbwe¹ na Mussa Omari Amanzi²

¹Shule ya Msingi Duthumi

²Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro

Ikisiri

Vitanzandimi ni nui muhimu ya fasihi simulizi. Nui hii ina mnasaba wa moja kwa moja na jamii kulingana na zama, itikadi pamoja na utamaduni wa jamii ikiwemo mila, dasturi, mtindo wa maisha, ufundi wa aina zote na kadhalika. Utanzu huu wa semi katika fasihi simulizi una kazi lukuki katika jamii, miongoni mwa kazi hizo ni kutoa motisha kwa wanafunzi kutamka maneno (Morris, 1975). Kadhalika, vitanzandimi huleta raha kwa watu kwa sababu ndani yake mna marudio ya sauti fulani ambazo huleta ladha ya kimuziki na hata pale msemaji anaposhindwa kuyatamka maneno hayo (Wanjala, 2011). Hata hivyo, vitanzandimi kama utanzu muhimu wa semi huiburudisha jamii hasa watoto (Wamitila, 2004). Licha ya umuhimu na kazi kubwa ifanywayo na vitanzandimi katika jamii, nui hii ya fasihi simulizi bado haijafafanuliwa kwa kiwango cha kutosha katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu ya kutoelezwa kwa uwazi sifa za maneno hayo (vitanzandimi) zaidi ya kudokezwa kijumla tu kupitia fasili zilizotolewa na wataalamu mbalimbali wa fasihi. Kadhalika, kumekuwa na utofauti na mwachano mkubwa wa mifano ya vitanzandimi kutokana na miegamo ya fasili za vitanzandimi zilizodokezwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi. Kwani, baadhi ya wataalamu huamini kuwa vitanzandimi ni mchezo wa maneno, wengine huamini ni maneno yanayotatiza kimatamshi, na wengine wakiamini ni maneno yanayokaribiana sana kimaana na kisauti pale yanapotamkwa. Ingawa si jukumu wala lengo la makala yetu kushughulikia utofauti ama mwachano huo wa mifano ya vitanzandimi kutokana na miegamo hiyo ya fasili za vitanzandimi zilizodokezwa na wataalamu wa fasihi 'la hashu'. Makala hii ilitia nanga katika kubainisha sifa zinazovitambulisha vitanzandimi vya Kiswahili katika mawasiliano ya jamii (watu). Hivyo, kupitia makala haya imebainika kuwa vitanzandimi vya Kiswahili vina sifa zake kadha wa kadha kutokana na uamilifu wake kwa jamii.

Maneno Muhimu: *Vitanzandimi, Fasihi Simulizi, Mawasiliano, Jamii, Kiswahili*

Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Makala imejielekeza zaidi katika kubainisha na kuzieleza sifa mbalimbali za vitanzandimi vya Kiswahili katika mawasiliano ya jamii. Hii ni kutokana na kubainika kwamba vitanzandimi vya Kiswahili vina sifa zake zinazovitambulusha ili vijulikane vema kwa jamii. Hata hivyo, yapo mambo kadhaa muhimu yaliyojadiliwa katika makala haya, miongoni mwa mambo hayo ni dhana ya vitanzandimi na mawasiliano ya jamii, utata wa istilahi zilizotumika kurejelea utanzu wa vitanzandimi, pamoja na sifa za vitanzandimi vya Kiswahili katika mawasiliano ya jamii. Kadhalika, makala imedokeza nadharia, njia zilizotumika katika utafiti, hitimisho na marejeleo yaliyotumika.

Makala haya yalitumia data za watu wanaoishi Tanga Mjini kutoka katika Jiji la Tanga, ambapo watoaarifa wake walipatikana kwa njia ya usaili. Data zilizokusanywa zilitokana na vitanzandimi vya Kiswahili vinavyotumiwa na jamii hiyo teule katika mawasiliano yao, ambapo zilikuwa ni baadhi ya vitanzandimi vya Kiswahili pamoja na baadhi ya sifa za vitanzandimi vya Kiswahili. Data zote zilitokana na watoaarifa wenyewe, ambapo nadharia ya *Fasihi Ina Kwao* ilitumika kuzichambua na kuzifafanua data hizo kutokana na misingi bora iliyojengwa na waitifaki wa nadharia hiyo akiwemo (Sengo, 2008, 2009; na Ntarangwi, 2004).

Dhana ya Vitanzandimi na Mawasiliano ya Jamii

Vitanzandimi ni sentensi au vifungu vya maneno ambavyo huwatatiza wasemaji wakati wa kuyasema maneno au sentensi hizo kwa haraka (tafsiri yangu). Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), vitanzandimi ni kauli zenye maneno yenye mchanganyiko au mfuatano wa sauti zinazotatanisha kuzitamka. Kwa mfano kusema “*Kupa mpe akupae kumpa asokupa si kupa ni kutupa*” (Mganga, 2021); Kadhalika neno *mawasiliano*, linarejelewa kama ni utaratibu wa kufikisha mawazo, taarifa na mitazamo kutoka kwa muanzilishi (msemaji) na kwenda kwa mpokeaji (msikilizaji) wa jambo kwa lengo la kushawishi kile kilichokusudiwa (Kiura na Munga, 2016). Pia, wanaeleza kuwa mawasiliano ni ile hali ya kupeana habari, maarifa, kuelezana hisia na kupeana ujuzi kwa kutumia ishara, maneno, picha na michoro. Hivyo, dhana ya ‘*mawasiliano ya jamii*’ iliyotumiwa katika utafiti wa makala hii imekusudiwa ile hali ya jamii au watu kama watumiaji wa lugha kufikishiana ujumbe, maarifa ama taarifa kupitia lugha wanazozitumia vikiwemo vitanzandimi vya Kiswahili ili kuelewana na kupatana katika mambo yao.

Utata wa Istilahi Zilizotumika Kurejelea Utanzu wa Vitanzandimi

Kuna maandiko mengi yaliyohusu maana za vitanzandimi, Wamitila (2004) ni miongoni mwa wataalamu waliotujua maana hizo. Mtaalamu huyu anatumia jina ‘vitanza ulimi’ kurejelea maana ya vitanzandimi kuwa ni vifungu vya maneno ambavyo huonesha mchezo mkubwa wa maneno yanayokaribiana kimaana na kisauti. Anaendelea kusema kuwa vifungu hivi huhitaji umakini mkubwa wakati wa kuvitamka hasa kutokana na mfanano wake wa karibu uliopo kati ya maneno na sauti zilizopo. Wamitila (2004) anasisitiza kwamba kitendo cha vifungu hivyo vya maneno kuutatiza au kuutanza ulimi ndio msingi wa kujulikana kwa jina hilo ‘*vitanza ulimi*’. Maelezo hayo yaliyosemwa na Wamitila hapo juu kuhusu vitanzandimi tuliona ni faafu zaidi, kwa sababu ya maneno yenyewe jinsi yalivyo na istilahi hiyo ‘*vitanza ulimi*’ iliyotumiwa na mtaalamu huyu kuwa na uhusiano mkubwa kimtazamo. Lakini pia, si rahisi kwa kila mtamkaji wa vitanzandimi kutamka bila kuutanza ulimi wake. Maana hiyo iliusaidia sana utafiti wa makala hii kulitumia jina hilo ‘*vitanza ulimi*’ kama msingi bora wa kuzitafuta data zilizohusu andiko letu ili kutimiza malengo tuliyojiwekea.

Kadhalika, Wamitila (2008) analitumia jina ‘tauria’ kurejelea maana ya vitanzandimi kuwa ni aina ya mchezo wa maneno kwa namna inayomfanya msemaji afasiri maana zaidi ya moja au mihusianisho mingine. Maana hii ya Wamitila (2008) pia iliufanikisha utafiti wa makala yetu kuitumia istilahi hiyo ili isaidie kupata marejeleo yaliyohusu mada hii. Japokuwa ilihitajika kwa mtaalamu huyu kwanza afafanue hili jina ‘tauria’ kwa kubainisha misingi, chanzo na asili yake, ili wasomaji waweze kuelewa kwa urahisi kwamba tunapozungumzia ‘tauria’ tunazungumzia kitu kitokacho sehemu kadha wa kadha na ijulikane pia kipo namna gani. Hata hivyo, hakuna sehemu yoyote katika andiko hilo iliyoonesha kuwa tauria hiyo imetokea wapi au ni kipera kitokacho katika tanzu gani ya fasihi (simulizi au andishi), tofauti na alivyoeleza Mulokozi (1996). Mulokozi (1996) yeje aliibainisha kabisa ‘kauli tauria’ kama utanzu wa semi katika fasihi simulizi.

Mulokozi (1996) naye analitumia jina ‘kauli tauria’ kurejelea maana ya vitanzandimi kuwa ni kauli zenye maneno yenye mchanganyiko au mfuatano wa sauti zinazotatanisha kuzitamka. Mulokozi akionesha kauli hizo zenye maneno yenye mchanganyiko na mfuatano wa sauti hizo zinazotatanisha kuzitamka (vitanzandimi) kwa kumnukuu Liyong (1972) kwa lugha ya Gikuyu kama ifuatavyo;

1. Gikuyu:

*Kaanaka Nikora kona kora kora, nako kora
kona kaana ka Nikora kora.*

(Taban Lo Liyong, 1972:157- 158)

Maneno hayo yaliyoelezwa kwa lugha hiyo ya Gikuyu yalimaanisha kwamba “*Kitoto cha Nikora kiliona kiluwiluwi (cha chura) kikakimbia, kiluwiluwi nacho kilipokiona kitoto (cha chura) pia kikakimbia*”. Kwa fasili hii mtaalamu huyu alitufungua macho kujua kwamba vitanzandimi pia ni aina ya sauti zinazotatanisha kuzitamka. Utata huo ni dhahiri unaonekana hapo juu katika mfuatano huo wa sauti ‘k’ na ‘n’ kama zinavyoonekana.

Vivyo hivyo, Mulokozi (2017) analitumia jina ‘vitae’ kurejelea maana ya vitanzandimi kuwa ni kauli zenye maneno yenye mchanganyiko au mfuatano wa sauti zinazotatanisha kuzitamka. Maana hii ilionekana kwenda sambamba na ile aliyoeleza yeye Mulokozi (1996) kwamba “kauli tauria ni kauli zenye maneno yenye mchanganyiko au mfuatano wa sauti zinazotatanisha kuzitamka”. Kiukweli istilahi zote mbili (kauli tauria na vitae) zilizotumiwa na Mulokozi (1996; 2017) ziliongeza upeo kwa mtafiti wa kuizamia kwa kina makala haya, hasahasa kujua maana nyingi za vitanzandimi kama zilivyotumika katika makala haya. Lakini pia, istilahi hizo zilitoa kibali kwa mtafiti cha kuyazamia mapitio mbalimbali bila ya kujali istilahi iliyochaguliwa kutumika katika makala haya ambayo ni ‘vitanzandimi’, badala ya nyingine nyingi kama zilivyoielezwa hapo juu na Wamitila (2004; 2008), pamoja na Mulokozi (1996; 2017).

Kadhali Samwel (2015), analitumia jina ‘vitanzandimi’ kuwa ni kipera kinachojumuisha maneno ambayo hutatiza kimatamshi yanapotamkwa kwa haraka. Samwel (ameshatajwa) aliendelea kutujua kuwa hivi vitanzandimi pia hujulikana kwa majina mengine kama ‘kauli tauria na mchezo wa maneno’. Samwel alikiri kuwa wataalamu wa fasihi wameyatumia majina hayo (kauli tauria na mchezo wa maneno) katika kazi zao za kifasihi, kama ambavyo mtafiti wa makala haya alivyojaribu kuyaonesha majina hayo kwa kuwanukuu baadhi ya wataalamu. Kiukweli, Samwel (2015) alitufumbua macho katika andiko letu hili kwa istilahi alizozionesha, kwani zilimuhamasisha mtafiti na hata kumpa nguvu ya kuzitumia istilahi hizo katika kuyazamia maandiko yaliyoihusu mada ya makala yetu ili kujenga vema. Ingawa Samwel ni kama alitutatiza kidogo katika maelezo yake pale aliporejelea vitanzandimi, aliposema “kitanzandimi ni kipera” lakini mtaalamu huyu hakuwabainishia wasomaji wake kuwa ni kipera kitokacho katika tawi gani la fasihi (simulizi au andishi?) ili wasomaji waweze kutambua vema. Kwa mawazo yetu, tunaona bora tungejuzwa mwanzoni kwamba kipera hiki hupatikana katika utanzu wa fasihi simulizi kama alivyotubainishia Mulokozi (1996).

Kwa ujumla, istilahi zilizotumika kurejelea vitanzandimi tulizikubali hasa kutokana na manufaa yake tuliyoyapata kama tulivyoyaeleza katika hoja zilizotangulia, lakini kwa mawazo yetu tunaona baadhi ya istilahi hizo huleta utata kwa wasomaji. Hii ni kutokana na kutokubainishwa misingi, asili na uchanganuzi mpana wa majina/istilahi hizo zilizotumika kurejelea utanzu huu wa ‘vitanzandimi’. Haitoshi tu mtu kujua maana ya ‘kitate’ bila ya kujuzwa msingi, asili na uchanganuzi wa istilahi yenyewe ‘kitate’ itumikayo katika andiko husika. Ingawa si jukumu la makala haya kuziba pengo hilo la kubainisha misingi, asili na uchanganuzi wa istilahi hizo zilizotumiwa na wataalamu kurejelea utanzu huu wa vitanzandimi. Lakini kwa mawazo yetu, tunaona istilahi ya ‘vitanzandimi’ ingefaa zaidi kuliko istilahi zilizotumiwa na baadhi ya wataalamu. Hii ni kwa sababu jina lenyewe lina mwitiko wa haraka katika dhana iliyokusudiwa ambayo ni maneno yanayosababisha mtataziko wa ulimi/ndimi. Hata hivyo, makala haya inakubaliana na istilahi ya jina ‘vitanzandimi’ kama ikiwa vitanzandimi hivyo ni zaidi ya kimoja, na istilahi ya jina ‘kitanza ulimi’ kama kitanzandimi husika kitakuwa ni kimoja, na wala sio kuzichanganya istilahi hizi ambatani zilizokaa katika hali ya umoja na wingi kwa kurejelea dhana moja ya ‘vitanzandimi’.

Pia kwa kuwa ni nomino ambatani ya jumla, kisarufi haipendezi kuwa ‘vitanza ulimi’. Neno *vitanza* ni wingi, hivyo hata neno *mwambata* linapendeza kuwa la wingi. Kwa ujumla istilahi hiyo huumana kimtazamo na uhalisia wa kauli hizo zinazotatiza ndimi za watu/wasemaji.

Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliozaa makala haya umeongozwa na nadharia ya *Fasihi Ina Kwao*, ambayo muasisi wake ni Sengo (2009). Katika miaka ya 1978 mwanataaluma na mwanajadiiya Sengo alianzisha nadharia hii ya ‘Fasihi Ina Kwao’ kutokana na nadharia nyingi zilizopo hasa za kutoka kwa waanzilishi wa Ughaibuni/Kimagaribi kuwa na kasumba za Kizungu. Nadharia hizo zilionekana kuwa na pengo la mashiko kwa Waafrika kutojivunia Uafrika wao. Hivyo, nadharia hii ya Fasihi Ina Kwao inaziba pengo hilo na kuwataka wanasanaa jadiiya kurejelea ujumi¹ wa Waafrika, yaani ujumi wa Mkwere,

¹ Ni tawi la falsafa linaloshughulika na dhana za uzuri, uchanya, ladha, ubora, uhasi na uwi/ubaya (Ameir, 2011; na Badru, 2015). *Uzuri*, ni ukamilifu wa hisia za akili unaoleta kulitazama jambo au mambo fulani katika mtazamo ‘chanya’.

Mbugu, Mkinga na wengine wote kuwa sanaa jadiiya yao ina thamani na mashiko katika jamii yao husika (Sengo, 1978).

Wazo kuu la nadharia hii ni kwamba, kila sanaa jadiiya ya jamii inafuata utamaduni wa jamii hiyo. Hii inamaana kwamba kila jamii ina jadi yake, yaani habari za Wapare ni habari za Wapare, haziwahusu Wabungu (Mlacha na wenzake, 1995; na Sengo, 2008). Ntarangwi (2004) akishadidiya maelezo ya wana taalimu wenzake anasema kuwa, mtunzi au mtoaji wa miiko ni mwana jamii. Mwana jamii huyu ana nafasi katika jamii husika na kwa hali hiyo hawezi kukwepa wajibu wake katika kulea na kufundisha maadili ya jamii yake. Misimamo ya Sengo katika nadharia hii ni kwamba, ili mtu aielewe fasihi simulizi ya jamii yoyote sharti akujuwe kule jamii hiyo inakoishi, utamaduni wao, mila zao, dasturi zao, ada zao, lugha zao na kadhalika. Anaendelea kusisitiza kuwa, ili mtu aieleze fasihi ya jamii fulani ni lazima mtu huyo kulijua eneo husika, mila, dasturi, silka, kaida na mema ya utamaduni wa jamii hiyo. Pia, alisema;

“Fasihi ya Kiswahili kwao ni Uswahilini, Pwani ya Mwambao wa Afrika Mashariki. Waswahili wana jadi zao, katika viambo vyao, miji yao, vijiji vyao, makaazi yao na kadhalika”.

Hivyo, lugha vikiwemo vitanzandimi vya Kiswahili, dasturi, mila, kazi, sanaa na jadi kuna vinakotoka, kila jamii ina matumizi ya lugha yake, desturi zake, mila zake, sanaa yake, kazi na jadi yake na hakuna ambayo ni bora zaidi ya nyingine.

Mawazo ya muitifaki Sengo na wafuasi wake kuhusu nadharia hii ya *Fasihi Ina Kwao* yalitujenga kuwa fasihi simulizi ina sifa zinazofanana duniani kote, na inapaswa kutambuliwa kuwa kila jamii ina fasihi yake ya kipekee. Jamii huasisi utamaduni na utamaduni humtambulisha mwanajamii. Utamaduni huibeba sanaa na sanaa ndiyo iundayo fasihi. Fasihi hujumuisha lugha na lugha ndiyo iliyobeba hivi vitanzandimi vya Kiswahili ambavyo ndani yake vimesheheni matumizi mbalimbali kwa jamii.

Nadharia ya Fasihi Ina Kwao imesaidia sana katika utafiti uliozaa makala haya kuangalia sifa za vitanzandimi vya kiswahili katika mawasiliano ya jamii. Vitanzandimi vya Kiswahili ni sehemu ya fasihi simulizi, ambavyo huchukua nafasi ya lugha na dasturi za jamii. Aidha, mawazo ya huyu muitifaki Sengo (2008; 2009) na wafuasi wake kuhusu nadharia hii teule yaliujengea nguzo muhimu utafiti wa makala hii, ambazo zilisimama kama mihimili ya kugemea katika utafiti wa makala yetu.

Mihimili hiyo ilisitiza kuwa, fasihi haiishi katika ombwe ina kwao, na kwao ni ndani ya jamii. Hivyo, uelezaji wa sifa za vitanzandimi vya Kiswahili katika kutimiza lengo la utafiti wa makala hii ulifanywa kwa kutumia maarifa na ujuzi wa wazawa wa jamii tafitiwa, ambayo ndiyo inayovitumia vitanzandimi hivyo vya Kiswahili.

Mbinu Zilizotumika Kukusanya Data

Utafiti uliozaa makala haya ulikuwa ni wa kitaamuli ambapo mwegamo wake ni wa kiufafanuzi kwa kuwa masuala ya tajriba, mahusiano, mila na dasturi na mitazamo ya watu ndiyo yaliyochunguzwa na kufafanuliwa (Kothari, 2009). Mbinu ya usaili ndiyo iliyotumika katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii imetumika katika kukusanya data za uwandani kwa kuwahusisha watafitiwa teule wenye uwezo wa kuvitumia vitanzandimi vya Kiswahili vizuri, wote hawa kutoka Tanga Mjini. Utafiti ulijiegemeza zaidi katika kupata taarifa za msingi kuhusu sifa za vitanzandimi vya Kiswahili kupitia vitanzandimi vya Kiswahili vinavyozungumzwa na jamii ya watu wanaoishi huko Tanga Mjini. Huko, vilibainika vitanzandimi vingi vya Kiswahili kutoka kwa jamii hiyo tafitiwa pamoja na kuelezwa dhima zake katika jamii. Baadhi ya vitanzandimi vilivyobainishwa na watafitiwa vimetumika katika makala haya kwa lengo la kushadidia hoja zilizotolewa na watafitiwa huko uwandani kuhusu sifa za vitanzandimi vya Kiswahili. Data zilizopatikana zilichanganuli na kuwasilishwa kwa usahihi ili kupata taarifa faafu

Haijalishi mwengine kulichukulia jambo hilo kimtazamo ‘hasi’, lakini pia mtazamo wake (hasi) hauondoi uzuri ‘chanya’ kwa atazamaye chanya.

za utafiti zilizo hitajika. Hivyo, makala imezichambua data hizo kwa usahihi ili kupatikana taarifa zenye tija kwa wasomaji.

Sifa za Vitanzandimi vya Kiswahili Katika Mawasiliano ya Jamii

Mbali na kubainika kwa dhima mbalimbali za vitanzandimi vya Kiswahili katika jamii kama ambavyo wataalamu wengi wamejaribu kueleza katika kazi mbalimbali za fasihi kuwa huburudisha, huelimisha, huongeza umahiri wa ujifunzaji lugha n.k. Lakini bado kuna umuhimu mkubwa wa kufahamika kwanza utanzu wenyewe kwa kubainisha sifa zake. Sifa za kitu au dhana ndio huweza kukipambanua kwa kukibainisha kitu au dhana hiyo. Zipo sifa tano zilizobainika katika vitanzandimi vya Kiswahili. Miongoni mwa sifa hizo ni kuwa huweza kuundwa kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi, hutumia maneno yenye maana zaidi ya moja, hutumia maneno yenye sauti sawa. Lakini pia, huundwa kwa maneno yenye mwitiko sawa kisauti mwishoni lakini maana tofauti, halikadhalika huundwa kwa kurudiwa silabi moja inayojitokeza mara nyingi katika maneno. Fasihi haiishi katika ‘ombwe’ ina kwao, na kwao ni ndani ya jamii. Jamii teule ya watu wa pwani ya Tanga Mjini kama watumiaji wa vitanzandimi vya Kiswahili ndiyo iliyotumiwa na makala haya kuzieleza sifa hizo za vitanzandimi vya Kiswahili kama ifuatavyo:

Huundwa kwa Sauti Zinazokaribiana Kimatamshi

Watafitiwa walieleza kuwa vitanzandimi vya Kiswahili vina sifa zake zinazovitambulisha kwa jamii, miongoni mwa sifa hizo zilizobainika ni kwamba vitanzandimi vya Kiswahili huundwa kwa sauti zinazokaribiana sana kimatamshi². Takribani vitanzandimi vingi vya Kiswahili vinavyotumika katika mawasiliano ya jamii zetu huwa na sauti zinazokaribiana sana kimatamshi. Hii ni kutokana na namna vitanzandimi hivyo kuwa na maneno yanayofuatana sana katika utamkwaji wake. Hili linadhihirika katika kitanzandimi cha Kiswahili kilichobainishwa na Mt1 huko uwandani. Kitanzandimi hicho kilifahamika kama ifuatavyo:

‘Bwaja mtatuzi tata, tatua tata tatuzi’

(Chanzo: Utafiti wa Uwandani, Machi 2022)

Katika kitanzandimi hicho tunayaona maneno kama ‘**mtatuzi**’, ‘**tata**’, ‘**tatua**’, ‘**tata**’, na neno ‘**tatuzi**’ namna yalivyochezewa na msemaji mpaka kuunda sauti zinazokaribiana sana kimatamshi. Maneno haya ‘**mtatuzi**’, ‘**tata**’, ‘**tatua**’, ‘**tata**’, na neno ‘**tatuzi**’ yametawaliwa na silabi ‘**ta**’ na ‘**tu**’ zenye ukaribu wa kisauti ambazo muunganiko wake ndio uliozaa ukaribu wa kimatamshi katika maneno haya ‘**mtatuzi**’, ‘**tata**’, ‘**tatua**’, ‘**tata**’, na neno ‘**tatuzi**’. Hivyo, tunaweza kusema kila kitu kina sifa inayokitambulisha ili kibainike kwa urahisi, sifa mojawapo ya vitanzandimi vya Kiswahili tunaweza kusema ni kule kuundwa kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi kama ilivyo katika vitanzandimi vyengine vinavyozungumzwa na jamii mbalimbali.

Data hiyo hapo juu haikupatikana katika ombwe, bali ilipatikana kupitia jamii iliyoteuliwa, yaani jamii ya watu wa pwani ya Tanga Mjini. Uamuzi uliopelekea kuteuliwa jamii hiyo ni nguzo bora iliyojengwa na nadharia ya Fasihi Ina Kwao kupitia msingi wake. Nadharia iliamini kwamba “Fasihi haiishi katika ombwe, ina kwao, na kwao ni ndani ya jamii”. Wazo hili ndilo lililomsukuma mtafiti kuchagua jamii ya watu wa pwani ya Tanga Mjini kama jamii teule katika utafiti wa makala haya. Vitanzandimi vya Kiswahili hutumiwa sana na jamii hiyo, hivyo jamii hiyo teule ilifaa zaidi kutujuza sifa za vitanzandimi vya Kiswahili.

Hutumia Maneno yenye Maana Zaidi ya Moja

Vitanzandimi kwa ujumla ni lugha ya mafumbo ambayo muda mwingine hutumika kwa lengo la kuficha jambo linalozungumziwa kuwa la siri, kwa maana ya kutofahamika na watu wengine wasiovielewa vyema vitanzandimi. Hali hiyo imepelekea vitanzandimi vingi vya Kiswahili kuwa na sifa ya kutumia maneno yenye maana zaidi ya moja³. Utafiti ulibaini kuwa, wafuatiliaji na wasikilizaji

²Hoja hii ilisemwa huko uwandani na Mt12 katika kitongoji cha Kiungani, Kata ya Mnyanjani Mjini Tanga 26/03/2022

³Hoja hii ilitolewa na Mt1 huko uwandani Machi 21, 2022 katika Kitongoji cha Ndaoya, Kata ya Chongoleani Mjini Tanga.

wengi wa vitanzandimi vya Kiswahili huwa hawaelewi vizuri maana za maneno yanayotumika katika vitanzandimi, hatimaye kushindwa kuelewa undani wa maudhui yabebwayo na vitanzandimi hivyo mpaka uwe mzawa wa lugha husika. Watu wengi hufikiri kwamba watumiaji vitanzandimi vya Kiswahili huvitumia kwa lengo la kuzipamba kazi zao au kufurahisha na kuburudisha tu mwishowe kushindwa kuzingatia maudhui yabebwayo na vitanzandimi hivyo. Katika dondoo hapo chini tunaona namna ambavyo Mt2 alivyojaribu kutumia kitanzaulimi cha Kiswahili ili kuonesha maneno yenye maana zaidi ya moja:

‘Yukupi akupae upo ungalipo huku tulipo ambapo sipo hapo ulipo upo wala ulipo Mtondoo?’.

Tafsiri:

*‘Yukowapi atakaekupa **upo** ikiwa wewe upo huku tulipo sisi ambapo sipo ulipo huo upo wala sipo ulipo **Mtondoo?**’.*

(Chanzo: Utafiti wa Uwandani, Machi 2022)

Katika kitanzaulimi hicho neno ‘**upo**’ lilikusudiwa ‘kifaa kinachotumiwa kuchotea maji au kukumbia maji kutoka kwenye chombo cha majini na kuyatoa nje’ na neno ‘**Mtondoo**’ lilitumika kama ‘jina la mtu aitwaye Mtondoo’. Ikiwa, neno hilo ‘*upo*’ katika jamii zetu limezoeleka kama ‘ishara ya uwepo wa mtu au kitu kuwa sehemu fulani’, kadhalika neno ‘*Mtondoo*’ ambalo pia hufahamika kama ‘bunduki ya zamani ambayo hufyatuliwa kwa kushindilia mafusho ya fataki’, pia hujulikana kama ‘ndoo ya kuhifadhia choo jela’. Kuelewa maana ya misamiati iliyotumika katika kitanzaulimi hicho kunahitaji weledi mkubwa wa kuifahamu sana lugha. Wasikilizaji wasiokuwa wazawa au wasipoweza kutumia ujuziwa lugha huishia kuona vitanzandimi vya Kiswahili kama ni burudani tu kumbe ndani yake mna maudhui yenye maana nzuri kwao. Hivyo, ujumbe lengwa unaachwa na kutomakinikiwa na hadhira iliyosikiliza kitanzaulimi hicho. Vitanzandimi vya Kiswahili kutumia maneno yenye maana zaidi ya moja ni kawaida, ili kujengwa utata wa kimatamshi na kimaana kwa jamii inayohusika.

Nadharia teule ya Fasihi Ina Kwao ilifaa sana katika utafiti wa makala hii. Nadharia hiyo iliamini kwamba fasihi yoyote inayotumika katika jamii ina kwao, na kwao ni ndani ya jamii husika iliyoizaa. Kwa jamii ya watu wa pwani ya Tanga mjini huweza kupata burudani katika kitanzaulimi hicho pamoja na kupata ujumbe uliokusudiwa. Waswahili wanasema “siri ya mtungi aijuae kata” na “aisifuye mvua imemnyeshea”. Isingekuwa rahisi kuzifahamu sifa za vitanzandimi vya Kiswahili kisawasawa kutoka katika jamii nyingine ikiwa watumiaji wake ni jamii ya watu wa pwani ya Tanga Mjini. Hivyo, mawazo ya nadharia hiyo teule ya Fasihi Ina Kwao yalimuongoza mtafiti wa utafiti huu kwamba ili azijue sifa za vitanzandimi vya Kiswahili kisawasawa ni lazima atangamane na jamii hiyo teule ili apate taarifa muhimu anazozitaka kama ambavyo imefanywa na mtafiti.

Hutumia Maneno yenye Sauti Sawa

Mt3 alieleza kuwa vitanzandimi vya Kiswahili ni sentensi ambazo huwa na sifa ya kuwa na maneno yenye sauti sawa. Mtafitiwa huyo alibainisha kuwa uwepo wa maneno yenye sauti sawa katika vitanzandimi vya Kiswahili ndio ambao humfanya mtumiaji wa kitanzaulimi husika aweze kutatazika kimatamshi. Katika kubainisha ukweli wa hoja yake hiyo hapo juu mtafitiwa alirejelea kitanzaulimi kisemacho:

‘Lilo silo lilo lilo ila lilo ndilo lilo lilo litakiwalo’

(Chanzo: Utafiti wa Uwandani, Machi 2022)

Katika kitanzaulimi hicho yanabainika maneno kadhaa yaliyokiunda, kwa mfano neno ‘**lilo**’. Neno hilo limejitokeza mara sita katika kitanzaulimi hicho likiwa na sauti sawa ambayo ni sauti ‘**lilo**’, likifuatiwa na maneno kama ‘**silo**’, ‘**ila**’ na neno ‘**litakiwalo**’ yenye sauti zinazotofautiana. Katika kitanzaulimi hicho cha Kiswahili tunaona neno kama ‘**lilo**’ lililojitokeza mara nyingi huku likiwa na sauti sawa pamoja na maneno kama ‘**silo**’, ‘**ila**’ na neno ‘**litakiwalo**’. Maneno hayo, yameunganishwakwa pamoja na kuunda kitanzaulimi hicho cha Kiswahili ambacho kutokana na

mseto huo wa maneno husababisha utanzaji mkubwa wa ndimi za wazungumzaji. Hivyo, tunaweza kusema kuwa sifa mojawapo ya vitanzandimi vya Kiswahili ni kule kuwapo kwa maneno yenye sauti sawa. Ingawa haitokei mara zote vitanzandimi vya Kiswahili kuundwa na maneo yenye sauti sawa lakini kwa kiasi kikubwa huwa hivyo kama tuonavyo katika kitanzaulimi cha Kiswahili hapo juu.

Jamii teule ya watu wa pwani ya Tanga Mjini wanakubaliana na sifa hii ya vitanzandimi vya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mtafiti alitoa uhuru kwa kila mwanajamii aliyelengwa kutoa taarifa za utafiti huu kupitia njia ya usaili.

Huundwa kwa Maneno yenye Mwitiko Sawa Kisauti Mwishoni lakini Maana Tofauti

Sentensi nyingi ambazo huwa na tabia ya kuutatiza au kuutanza ulimi wakati wa utamkaji, zimebainika kuwa na maneno yenye mwitiko unaofanana kisauti mwishoni lakini maana za maneno yake hutofautiana. Hoja hii ilibainishwa na Mt4 huko uwandani alipotujuza kuhusu sifa za vitanzandimi vya Kiswahili. Mtafitiwa huyo alisema kuwa vitanzandimi vya Kiswahili huundwa kwa sifa nyingi ikiwamo matumizi ya maneno yenye mwitiko sawa kisauti lakini maana huwa zinatofautiana. Hili lilibainika katika kitanzaulimi kisemacho:

'Kuli fedhuli kali kwa kauli akila hula kwa ukali'

(Chanzo: Utafiti wa Uwandani, April 2022)

Katika kitanzaulimi hicho mtafitiwa alitoa ufafanuzi kwamba maneno '**Kuli**', '**fedhuli**', '**kali**', '**kauli**', '**akila**', '**hula**' na neno '**ukali**' ni jumla ya maneno yaliyounda kitanzaulimi hicho (hapo juu). Maneno kama '**kuli**', '**fedhuli**', '**kali**', '**kauli**' na neno '**ukali**' ndiyo ambayo huonesha mwitiko huo wa sauti sawa mwishoni, ambayo ni sauti '**li**' katika kila mwisho wa neno. Pia katika kitanzaulimi hicho lipo neno kama '**akila**' na neno '**hula**' ambayo pia huitikia sauti moja mwishoni, ambayo ni sauti '**la**'. Mt4 alidai kuwa mwitiko wa sauti hizo mwishoni mwa maneno hayo ndio unaosababisha mchengo/utatizaji mkubwa wa ndimi za watu pale yanapotamkwa kwa haraka maneno hayo. Mtafitiwa alisema, ingawa maneno hayo huitika kwa mwitiko wa sauti sawa mwishoni lakini maneno yake huitika kwa maana zinazotofautiana kama ilivyo kawaida ya vitanzandimi vya Kiswahili. Hivyo, tunaweza kusema kuwa vitanzandimi vya Kiswahili hujengwa na sifa hiyo ya kuundwa na maneno yenye mwitiko sawa wa sauti mwishoni lakini maana tofauti, ambapo ni tofauti na kauli nyingine zisizo vitanzandimi.

Hivyo, ili tuzijue sifa za vitanzandimi vya Kiswahili ililazimika kuiuliza jamii kama ambavyo utafiti huu umefanya. Mtafiti aliandaa maswali yake kwa jamii ya watu wa pwani ya Tanga mjini, hatimaye kupitia jamii hiyo imewezekana kuibuliwa sifa hii ya vitanzandimi vya Kiswahili kama ilivyoelezwa.

Huundwa kwa Kurudia Silabi Moja Inayojitokeza Mara nyingi katika Maneno

Vitanzandimi vya Kiswahili ili viweze kujenga utata wa kimatamshi katika ndimi za wazungumzaji wake ni lazima pawepo na uradidi wa silabi moja inayojitokeza sana katika maneno yanayotumika⁴. Uradidi huo wa silabi moja inayojitokeza mara nyingi katika maneno ndio ambao huwafanya wazungumzaji wengi wa vitanzandimi vya Kiswahili kutatazika pale wanapovitamka vitanzandimi hivyo. Hili linadhihirika katika kitanzaulimi kilichobainishwa huko uwandani na Mt5, kisemacho:

'Maajabu ya Mwajabu wa mzee Rajabu kuzaa mtoto kwa tabu leo kumuona ajabu'.

(Chanzo: Utafiti wa Uwandani, April 2022)

Katika kitanzaulimi hicho tunaona namna silabi '**bu**' ilivyojitokeza mara nyingi katika neno **Maajabu, Mwajabu, Rajabu, tabu** na neno **ajabu**, ambapo silabi hiyo inapoungana na maneno hayo yenye utofauti wa kimaana na kimatamshi husababisha sauti zinazoleta utanzaji mkubwa wa ndimi za wazungumzaji. Kwa mfano sauti za maneno '**Maajabu**', '**Mwajabu**', '**mzee**', '**Rajabu**', '**kuzaa**',

⁴Hoja hii ilitolewa na Mt15 huko uwandani Aprili 02, 2022 katika Kitongoji cha Vibambani, Kata ya Masiwani Mjini Tanga.

‘mtoto’, ‘tabu’, ‘leo’, ‘kumuona’ na neno ‘ajabu’ ambazo hukaribiana na hutofautiana kimatamshi. Ukaribu na utofauti huo wa sauti ambao hutokana na maneno hayo ndio unaozaa kitanza ndimi kama tunavyoona katika kitanza ndimi teule hapo juu. Hivyo, tunaweza kusema kuwa vitanzandimi vya Kiswahili vina sifa zake zinazovijenga ikiwemo hii sifa yakurudia silabi moja inayojitokeza mara nyingi katika maneno kama tulivyoona katika kitanzaulimi husika.

Nadharia yetu ya Fasihi Ina Kwao imechangia pakubwa katika utafiti huu, kwani ilitoa nafasi kubwa kwa watafitiwa (watu wa pwani ya Tanga Mjini) ambao ndio jamii lengwa kueleza namna wao wanavyovitumia vitanzandimi vya Kiswahili katika mawasiliano yao. Wanajamii wa pwani hiyo ndio waliotueleza kwamba vitanzandimi vya Kiswahili vina sifa ya kuundwa kwa kurudia silabi moja inayojitokeza mara nyingi katika maneno.

Hitimisho

Kama tulivyoeleza hapo awali kuwa makala hii imelenga kuzibainisha sifa za vitanzandimi vya Kiswahili katika jamii kama zilivyoenezwa hapo juu, lengo ziweze kutambulika kwa uwazi sifa za maneno hayo katika jamii. Hii ni kutokana na kukosa maandiko yanayozibainisha sifa za vitanzandimi vya Kiswahili kwa uwazi, licha ya kuwa maneno hayo (vitanzandimi) huzungumzwa sana na jamii zetu. Wataalamu wengi waliofasili maana za vitanzandimi ni kama walidokeza tu sifa za maneno hayo kijumla kupitia fasili walizozitoa katika maandiko yao, lakini hawakubainisha kwa uwazi sifa hizo ili jamii iweze kuzitambua. Hali inayopelekea wasomi na wahakiki wa kazi za fasihi kutozitambua sifa za vitanzandimi kwa uwazi. Ili kuondoa mazonge hayo, utafiti wa makala haya umebainisha sifa tano za vitanzandimi vya Kiswahili kama tuonavyo hapo juu. Ingawa si kweli kwamba makala haya imeweka ukomo katika kuelezwa sifa za vitanzandimi ‘la hashu’. Vitanzandimi ni lugha inayozungumzwa na jamii tofautitofauti, hivyo ni ruksa kwa waandishi wengine kuzama zaidi ili kuibua sifa nyingine za vitanzandimi ambazo inawezekana hazikudokezwa katika makala haya.

Marejeleo

- Ameir, Z.T. (2011). Ujumi wa Kisanaa katika Riwaya Teule za Mohamed Said Abdulla (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri). Chuo cha Sanaa, Lugha na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma (Haijachapishwa).
- Badru, Z.A. (2015). Taswira na Mabadiliko ya Kijumla Katika Vitendawili: Mfano wa Vitendawili vya Kiswahili. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu). Chuo cha Sanaa, Lugha na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma (Haijachapishwa).
- Kiura, M.K., & Munga, C.M. (2016). *Fundamentals of Communication Skills*. Mombasa: Kenya. Cactus East Afrika.
- Liyong, (1972). *Popular Culture in East Afrika*. Nairobi: Longman.
- Mganga, N.A. (2017). *Kifani cha Fasibi Neni*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers
- Mlacha, S.A.K., & wenzake. (1995). *Historian na Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam University Press.
- Morris, W. (1975). *The American Heritage of the English Language*. Boston: American Heritage Publishing Co. Inc
- Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasibi ya Kiswahili*. Dar Es Salaam: Moccony Printing
- _____. (1996). *Utangulizi wa Fasibi ya Kiswahili*. Dar Es Salaam. TUKI
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasibi*, Augustana College: Rock Island.
- Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasibi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Meveli Publishers (MVP).
- Sengo, T.S.Y. (2009). *Sengo na Fasibi za Kinchi*. Dar es Salaam: Al- Amin Education and Research Academy.
- _____. (2008). *Tafakuri ya Utu na Uhai*. Dar es Salaam: Huda Publishers.
- _____. (1978). “Utangulizi” katika Kandoro, S.A. *Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili na Lugha Yake*. Dar es Salaam: Longman
- Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasibi*. Dar es Salaam: Vide~ Muwa Publishers Limited.
- _____. (2004). *Kichocheo cha Fasibi Simulizi na Andishi*. Dar es Salaam: Focus Publication Limited.
- Wanjala, F.S. (2011). *Kitovu cha Fasibi Simulizi*. Mwanza, Tanzania: Serengeti Book Shop.